



NISHATI

HABARI ZA
NISHATI

News **Bulletin**

www.nishati.go.tz [Wizara ya Nishati](#) [wizara_ya_nishati_tanzania](#) [@Nishati2017](#) [Wizara ya Nishati](#)

Toleo Namba 20

Novemba 1-30, 2020

UMEME NDANI YA SIKU 21 - DKT. KALEMANI



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (mwenye miwani) alipotembelea kiwanda cha kuzalisha mita za LUKU cha Multicable ltd, kilichopo katika Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam, akiwa pamoja na viongozi mbalimbali wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na wamiliki wa kiwanda hicho.

UK.
2

JNHPP na matokeo chanya katika Uchumi wa Tanzania

UK.
6



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma

UMEME NDANI YA SIKU 21 - DKT. KALEMANI

Hafsa Omar-Dar es Salaam

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemmani ametoa agizo kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wakala wa Nishati Vijijini (REA) pamoja na wakandarasi wote kuhakikisha kuwa wananchi wote waliolipia huduma ya umeme wanaunganishiwa umeme ndani ya siku 21.

Alitoa agizo hilo Oktoba 5, 2020 wakati akiwa kwenye ufunguzi wa kiwanda cha kuzalisha mita za LUKU cha Multicable Ltd kilichopo katika Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam.

Dkt. Kalemmani alisema kuwa, wananchi takribani 5000 nchini wamelipia huduma hiyo na hadi sasa hawajaunganishiwa na huduma ya umeme ambayo ni muhimu katika kukuza

uchumi wa mtu mmoja mmoja na nchi kwa ujumla.

“Nimeshaeleza hapo mwanzo kuwa, hakuna tena sababu ya kuwacheleweshea wananchi kupata umeme kwa kisingizio cha uhaba wa mita za LUKU, kwenye kiwanda hiki ambacho nimekifungua leo kuna takribani mita za LUKU 500,000 ambazo zipo tu hata hazijanunuliwa.” Alisema Dkt. Kalemmani

Dkt. Kalemmani, alieleza kuwa, uwepo wa viwanda vingi vya ndani ambavyo vinazalisha vifaa vya usambazaji wa umeme kunarahisha usambazaji wa nishati hiyo, hivyo hakuna tena sababu itakayopelekea ucheleweshaji wa uunganishaji umeme kwa wananchi.

Pia, aliwataka wakandarasi wanaotekeleza mradi wa



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemmani (mwenye miwani) alipotembelea kiwanda cha kuzalisha mita za LUKU cha Multicable Ltd, kilichopo katika Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam, akiwa pamoja na viongozi mbalimbali wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na wamiliki wa kiwanda hicho.

usambazaji umeme vijijini kukamilisha kazi zao ifikapo tarehe 15 Oktoba mwaka huu, kwakuwa vifaa vyote vinavyohitajika kwa ajili ya usambazaji umeme vinapatikana kwenye viwanda vya ndani kwa bei rahisi na ubora wa juu.

“Wakandarasi wote ambao miradi yao imekaribia kukamilika ambao wengi wao wamebakiza vijiji viwili au vitatu, wakamilishe kazi zao kwa haraka na hatutawaongezea muda hivyo ifikapo Oktoba 15

mwaka huu wakabidhi miradi yao.” Alisema

Aidha, aliwataka wananchi wote ambao hawajafikiwa na huduma ya umeme kwenye maeneo yao, watulie na kuamini serikali yao kwani tayari Serikali imeshatekeleza miradi mingi na lengo ni kuhakikisha kuwa, umeme unafika kwa wananchi wote ambao hawajafikishiwa umeme ndani ya miaka miwili

INAENDELEA UK.

4



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemmani (mwenye miwani) akikata utepe kuashiria kwa ufunguzi wa kiwanda cha kuzalisha mita za LUKU, cha Multicable Ltd, kilichopo katika Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemmani (mwenye miwani) alipotembelea kiwanda cha kuzalisha mita za LUKU cha Multicable Ltd, kilichopo katika Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam, akiwa pamoja na viongozi mbalimbali wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na wamiliki wa kiwanda hicho.



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Mhandisi Zena Said
(Katibu Mkuu)

Makamu Mwenyekiti

Mhandisi Leonard Masanja
(Naibu Katibu Mkuu)

Mhariri

Veronica Simba

(Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini)

Waandishi

Veronica Simba

Teresia Mhagama

Zuena Msuya

Hafsa Omar

Msanifu Kurasa

Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano
Mtumba Dodoma, S.L.P.
2494, Dodoma

www.nishati.go.tz

[Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara ya Nishati)

[@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017)

[wizara_ya_nishati_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania)

[Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara ya Nishati)

KUUNGANISHIWA UMEME NDANI YA SIKU 21 KUTAONGEZA IDADI YA WENYE UMEME NCHINI

Hivi karibuni, Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani alitoa agizo kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wakala wa Nishati Vijijini (REA) pamoja na wakandarasi wote wa umeme nchini kuhakikisha kuwa wananchi wote waliolipia huduma ya umeme wanaunganishiwa umeme ndani ya siku 21.

Dkt. Kalemani alitoa kauli hiyo wakati akizindua kiwanda cha kuzalisha mita za Luku cha Multicable Ltd kilicho wilayani Temeke, jijini Dar es Salaam.

Alitoa agizo hilo baada ya kueleza kuwa, wananchi takribani 5000 nchini wamelipia huduma hiyo na hadi sasa hawajaunganishwa na huduma ya umeme.

Dkt. Kalemani alitoa agizo hilo kutokana na ukweli kuwa, kwa sasa vifaa vingi vya umeme vinazalishwa na kupatikana nchini ikiwemo nguzo, transfoma, nyaya na mita za Luku.

Kwa mfano, siku ya ufunguzi wa kiwanda hicho cha mita za Luku, kulikuwa na takribani mita 500,000 ambazo zilikuwa zikisubiri kununuliwa.

Dkt. Kalemani alitanabaiha kuwa, uwepo wa viwanda vingi vya ndani ambavyo vinazalisha

vifaa vya usambazaji wa umeme kunarahisha usambazaji wa nishati hiyo, hivyo hakuna tena sababu ya kuwachelewesha wananchi kupata umeme.

Ikumbukwe kuwa, nchi ya Tanzania tayari imeingia katika uchumi wa kati na nishati ni muhimu katika kuendesha uchumi huu, hivyo wananchi wote waliolipia huduma ya umeme wakiunganishwa na huduma husika ndani ya siku 21, ina maana wananchi wengi zaidi watakuwa na uwezo wa kutumia umeme kwa shughuli mbalimbali.

Tunasema Nishati ya umeme ni muhimu katika uchumi huu wa kati kwa sababu inapelekea ukuaji wa shughuli mbalimbali ikiwemo za kiuchumi mfano kwa kutumia nishati hiyo wananchi wataweza kuanzisha viwanda vidogo na vikubwa vya kuzalisha bidhaa zikatazouzwa ndani na nje ya nchi na hivyo kuongeza kipato cha mwananchi mmoja mmoja na nchi kwa ujumla.

Hivyo, agizo hili la Waziri wa Nishati halinabudi kutekelezwa kwa ufanisi ili kuongeza idadi ya wananchi wanaotumia umeme ambao utapelekea pia kuongezeka kwa shughuli za kimaendeleo zitakazowaongeza kipato wananchi.

Katunika Ki-nishati

WIZARA YA NISHATI
HAFLA YA UTIAJI SAINI WA MAKUBALIANO
YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA BOMBA
LA MAFUTA KUTOKA HOIMA NCHINI
UGANDA HADI BANDARI YA TANGA
NCHINI TANZANIA.
(CHATO, SEPTEMBER 13, 2020)



UMEME NDANI YA SIKU 21 - DKT KALEMANI

INATOKA UK.

2

ijayo.

Alieleza kuwa, Serikali imejipanga vizuri kuhakikisha huduma ya umeme inapatikana nchini kote na kuwataka wawekezaji nchini kuendelea kufungua viwanda vingi zaidi vya vifaa vya usambazaji wa umeme kwani kutarahisisha kupatikana kwa umeme kwa muda mfupi zaidi.

Alisema, Serikali itahakikisha inavilinda viwanda vyote vya kuzalisha mita za LUKU nchini ambavyo mpaka sasa vimefunguliwa viwanda takribani 10, ambavyo vinasaidia kutoa ajira nyingi kwa watanzania na Serikali imejipanga kuhakikisha inavilinda viwanda hivyo kwa kuwatafutia soko la kuuzia bidhaa zao.

Pia, aliwashukuru wawekezaji wa viwanda vya kutengeneza vifaa vya kusambazaji umeme nchini, ambavyo vimesaidia



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akizungumza wakati wa ufunguzi wa kiwanda cha kuzalisha mita za LUKU cha Multicable ltd, kilichopo katika Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam.

kutatua changamoto ya upatikanaji wa vitendea kazi vya usambazaji umeme

nchini.

Katika hatua nyingine, Waziri wa

Nishati, aliwahasisha wawekezaji mbalimbali nchini kuendelea kuwekeza katika viwanda vya kuzalisha mita za kusambazaji gesi majumbani.

Alieleza kuwa, ifikapo Januari mwaka 2021, wakandarasi wote watakapewa kazi ya usambazaji gesi majumbani hawataruhusiwa kuagiza mita kutoka nje ya nchi ili kulinda soko la ndani.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa kiwanda cha Multicable Ltd, Murtaza Alibhai alisema kuwa, wameamua kutekeleza sera ya Serikali ya Awamu ya Tano, ya Tanzania ya viwanda kwa vitendo ili kuendana na kasi ya ukuaji wa uchumi nchini, ambapo alisema kiwanda hicho mpaka sasa kimeajiri zaidi ya wafanyakazi 700.

Alisema kiwanda hicho kitahakikisha kuwa kinazalisha bidhaa bora zenye viwango vya hali ya juu ili kuchangia uchumi kupitia sekta ya viwanda.

Aidha, alieleza kuwa kampuni hayo inatarajia kuanzisha kiwanda cha kutengeneza transformo hivi karibuni ili kuhakikisha kuwa usambazaji umeme nchini unafanyika kwa haraka na watanzania wote wanafurahia kupata huduma ya umeme.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (mwenye miwani) alipotembelea kiwanda cha kuzalisha mita za LUKU cha Multicable ltd, kilichopo katika Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam, akiwa pamoja na viongozi mbalimbali wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na wamiliki wa kiwanda hicho.

HABARI KATIKA PICHA



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (mwenye miwani katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wa Taasisi za Wizara ya Nishati na viongozi mbalimbali wa kiwanda cha Multicable ltd, kilichopo katika Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa kiwanda cha kuzalisha mita za LUKU cha Multicable ltd, kilichopo katika Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam, Murtaza Alibhai akizungumza wakati wa ufunguzi wa kiwanda hicho, Oktoba 5, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (mwenye miwani katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wafanyakazi wa kiwanda cha kuzalisha mita za LUKU cha Multicable ltd, kilichopo katika Wilaya ya Temeke jijini Dar es Saalam.

JNHPP na matokeo chanya katika Uchumi wa Tanzania



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, akizungumza na Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara husika (kulia) pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (kushoto), wakati Ujumbe huo ulipozuru Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani ili kujionea maendeleo yake, Oktoba 03, 2020.

Na Mwandishi Wetu

Kutekelezwa kwa Mradi wa Kufua Umeme wa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) utakaozalisha megawati 2115, kunaleta matokeo chanya katika uchumi wa Tanzania.

Licha ya kuzalisha ajira kwa watanzania

wanaofanya kazi mbalimbali kwenye mradi huo, mradi husika utakapokamilika unatarajiwa kuzalisha umeme utakaopelekea nchi kuwa nishati ya umeme ya kutosha na ya gharama nafuu.

Licha ya upatikanaji wa umeme wa kutosha na gharama nafuu, mradi huo una manufaa mengine mbalimbali na

mojawapo ni Mkataba wa mradi huo unamtaka Mkandarasi kutumia malighafi zinazopatikana nchini na vifaa mbalimbali kutoka viwanda vya ndani hivyo kufungua fursa kwa wawekezaji na viwanda vya Tanzania.

Aidha, hadi kukamilika kwa utekelezaji wa mradi inatazamiwa kutumika tani 850,000 za simenti, tani 70,000 za nondo na

tani 250,000 za madini aina pozolani. Vyote hivyo vinatoka katika viwanda vya hapa nchini.

Vilevile, licha ya kutumia vifaa vinavyopatikana ndani ya nchi, Serikali imeendelea kuwaamini na kuwapa dhamana wataalamu wa

INAENDELEA UK.

7



Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REB), wakikagua miundombinu mbalimbali inayoendelea kujengwa katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani. Ujumbe huo ulitembelea Mradi husika, Oktoba 03, 2020 ili kujionea maendeleo yake.

JNHPP na matokeo chanya katika Uchumi wa Tanzania



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati), akiwa na Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REB), wakati Ujumbe huo ulipotembelea Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani, Oktoba 03, 2020 ili kujionea maendeleo yake.

INATOKA UK.

6

kitanzania katika usimamizi na utekelezaji wa mradi wa Julius Nyerere.

Mhandisi Said Kindamba, Meneja Ujenzi Mradi wa Julius Nyerere anaeleza kuwa, katika utekelezaji wa mradi huo, eneo la kuchepusha maji ya mto Rufiji (diversion tunnel) ni eneo muhimu kwani ndilo litakaloweza ujenzi wa bwawa.

"Kumbuka huu mradi ni wa kujenga bwawa la Julius Nyerere kwenye mto Rufiji, mto tayari upo na maji yanapita, ili kuweza kujenga bwawa inabidi hayo maji tuyatafutie njia mbadala na



Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REB), wakikagua miundombinu mbalimbali inayoendelea kujengwa katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani. Ujumbe huo ulitembelea Mradi husika, Oktoba 03, 2020 ili kujionea maendeleo yake.

INAENDELEA UK.

8

INATOKA UK.

7

njia hii ndio hili handaki la kuchepusha maji." alisema Mhandisi Kimbanga.

Anaongeza kuwa, wataalamu waliamua kuchoronga mwamba ili maji yapite ndani kuliko kuchimba kwenye mlima ambapo ingekuwa ni gharama kubwa na ingechukua muda mrefu kumalizika kuchimba na kuruhusu maji.

Anaeleza kuwa, zoezi linaloendelea ni uimarishaji wa mwamba ambapo zoezi hilo limefikia zaidi ya asilimia 42.

Mradi wa Julius Nyerere utakuwa na mashine tisa ambapo kila moja itatoa Mw 235, na hivyo jumla zitazalisha megawati 2115.

Kwa upande wa msimamizi wa mradi, Kampuni ya kitanzania ya TECU ndiyo inayojishugulisha na kusimamia mkataba kati ya TANESCO na Mkandarasi.

JNHPP na matokeo chanya katika Uchumi wa Tanzania



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REB) baada ya Ujumbe huo kuhitimisha ziara yake katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani, Oktoba 03, 2020, iliyolenga kujionea maendeleo yake.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (Rural Energy Board – REB), Wakili Julius Kalolo, akizungumza neno, wakati Bodi hiyo (kushoto) na Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati (kulia), walipotembelea Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji, mkoani Pwani, Oktoba 03, 2020 ili kujionea maendeleo yake. Wa kwanza kushoto ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja. PICHA ZOTE UK. 6,7&8 KUTOKA MAKTABA

DKT. KALEMANI AAGIZA UMEME USIKATWE WAKATI WOTE

Hafsa Omar-Dar es Saalam

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na wakandarasi wote nchini kusimamia ipasavyo upatikanaji wa umeme wa uhakika wakati wote ikiwemo kipindi chote cha uchaguzi.

Alitoa agizo hilo, Oktoba 17, 2020 wakati

akizungumza na waandishi wa habari, mara baada ya kumaliza kufanya ukaguzi wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme kilichopo Dege, Wilaya ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

“Nitoe rai kwa mameneja wote wa Tanesco, mhakikishe kuwa umeme haukatiki wakati wote na katika kipindi cha uchaguzi, tunataka wananchi wapige kura bila ya kero yoyote ya umeme.” Alisema Alisema, Serikali

inataka wananchi wafanye uchaguzi bila ya kujitokeza kwa changamoto yoyote inayotokana na umeme na kuwataka mameneja wote wa Tanesco kulisimamia agizo hilo.

Alisema kuwa, umeme unapopatikana katika muda wote, wananchi watatumia nishati ya umeme katika kujiletea maendeleo kwenye maeneo yao.

Kuhusu matumizi ya nguzo za zege, alisema kuwa zitasaidia na kupunguza kero ya

kukatika kwa umeme nchini kwakuwa nguzo hizo zinaweza kukaa kwa muda mrefu bila ya kuharibika.

“Ili wananchi waendeleo kuwa na uhakika wa umeme lazima tutumie nguzo za zege, kwa sababu maeneo mengine jijini Dar es Salaam umeme unakatika kwasababu wataalamu wetu

INAENDELEA UK.

10



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (mwenye miwani), Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi, Innocent Luoga (kulia) Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt. Tito Mwinuka (wa pili kushotokushoto) pamoja na wataalam mbalimbali wakiwa kwenye eneo ambalo nguzo za zege zimehifadhiwa ambazo zitatumika kwenye mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza Umeme kinachojengwa Dege, wilayani Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

DKT. KALEMANI AAGIZA UMEME USIKATWE WAKATI WOTE



Nguzo za Zege ambazo zinatarajiwa kutumika katika ujenzi wa mradi wa kituo cha kupoza umeme kilichopo Dege, Wilaya ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

INATOKA UK.

9

wanafanya marekebisho mara kwa mara yakiwemo ya kuondoa na kubadilisha nguzo zilizoharibika kwahiyo tukishaweka nguzo za zege tatizo hili

litamalizika."Alisema Dkt Kalemani.

Aidha, alieleza kuwa tayari nguzo za zege zimeanza kusimikwa katika maeneo mbalimbali nchini na maeneo ambayo yamepewa kipaumbele kwa kuanza kutumika kwa nguzo

hizo ni pamoja na sehemu ambazo kuna majaruba au maeneo ambayo kuna majimaji ambapo nguzo zinazotokana na miti zinaharibika kwa haraka.

Katika ziara hiyo, Waziri wa Nishati aliambatana na Kamishna Msaidizi wa Umeme

Mhandisi, Innocent Luoga, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt. Tito Mwinuka, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijiji (REA), Mhandisi Amos Maganga na waatalam mbalimbali kutoka Tanesco.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kuwasili katika ujenzi wa kituo cha kupoza umeme kilichopo Dege, Wilaya ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akizungumza na waandishi wa habari mara baada kumaliza kufanya ukaguzi wa kituo cha kupoza umeme kilichopo Dege, Wilaya ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

Mkandarasi wa REA atakiwa kumaliza vijiji vilivyosalia Gairo



Wataalam kutoka Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), wakikagua baadhi ya vifaa vya mkandarasi anayetekeleza mradi wa usambazaji umeme vijijini katika wilaya ya Gairo, mkoani Morogoro, wakati walipofanya ziara ya kukagua utekezaji wa mradi wa usambazaji wa umeme Wilayani Gairo.

Na Zuena Msuya, Morogoro

Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania

(TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), imemtaka Mkandarasi anayetekeleza mradi wa usambazaji umeme vijijini katika wilaya ya Gairo, mkoani Morogoro, kukamilisha kazi ya kufunga transfoma na kuunganisha wateja katika vijiji 14 vilivyosalia katika kusambaziwa umeme kati ya vijiji 32 vilivyopangwa kusambaziwa umeme.

Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Mbadala wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Christopher Nyondo, alieleza hayo wakati wa ziara ya wataalamu ya kukagua utekezaji wa mradi wa

usambazaji wa umeme wilayani Gairo, iliyofanyika hivi karibuni, kwa lengo la kuyapatia ufumbuzi

malalamiko ya wananchi waliyoyawasilisha katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Gairo na Mkuu wa

INAENDELEA UK.

13



Msimamizi wa usambazaji wa umeme vijijini katika Kanda ya Kati, kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Ahmed Chinemba, akiwaeleza jambo wataalam kutoka Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), wakati wa ziara ya kukagua utekezaji wa mradi wa usambazaji wa umeme wilayani Gairo, mkoani Morogoro.

Mkandarasi wa REA atakiwa kumaliza vijiji vilivyosalia Gairo

INATOKA UK.

12

Mkoa wa Morogoro kuhusu kusuasua kwa mradi huo.

Mhandisi Nyondo alisema kuwa, miongoni mwa malalamiko hayo ni pamoja na Mkandarasi kutokamilisha kazi za mradi

kwa wakati katika vijiji vilivyopangwa kupatiwa umeme kupitia mradi huo.

Vilevile alieleza kuwa, katika ziara hiyo Wataalam walipata fursa ya kutembelea maeneo ya vijiji vinavyolalamikiwa kwa kurukwa na kufanya mazungumzo na baadhi ya Wananchi ili kusikiliza kero na madai ya kutohusishwa

na wigo wa mradi, licha ya vijiji kuwepo kwenye mpango wa kupatiwa umeme katika mradi wa REA mzunguko wa Pili.

Alitaja Vijiji hivyo kuwa ni pamoja na Kinyolisi Mkwajuni, Kinyolisi Temeke, Kilama Chumila na Mnjilili Gairo.

Katika kumaliza malalamiko hayo, Mhandisi

Nyondo aliwaelekeza TANESCO na REA, kufikisha miundombinu ya umeme katika vijiji hivyo ifikapo Oktoba, 2020.

Vilevile aliagiza TANESCO kutoa elimu ya matumizi bora ya

INAENDELEA UK.

14



Baadhi ya miundombinu ya umeme ikiwa imesambaa katika baadhi ya nyumba za wakazi wilayani Gairo. Taswira hii ilichukuliwa wakati Wataalam kutoka Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) walipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa umeme wilayani humo hivi karibuni.

Mkandarasi wa REA atakiwa kumaliza vijiji vilivyosalia Gairo

INATOKA UK.

13

umeme na kuandikisha wateja wapya katika vijiji 14 vinavyofanyiwa kazi na Mkandarasi ikiwa ni maandalizi ya zoezi la kuunganisha huduma ya umeme kwa wateja wapya.

Kwa upande wao, REA na TANESCO waliahidi kuwa kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo, itakamilika kabla ya muda uliopangwa na kwamba wataendelea kumsimamia mkandarasi ili aongeze kasi ili kukamilisha mradi huo kwa wakati.



Baadhi ya Vifaa vya mkandarasi anayetekeleza mradi wa usambazaji umeme vijijini katika Wilaya ya Gairo, mkoani Morogoro.



Diwani wa Kata ya Gairo, wilayani Gairo mkoani Morogoro, Danistan Mwegoha, (katikati), akiwaonyesha Wataalam kutoka Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), sehemu ambayo miundombinu ya umeme ilipoishia katika eneo lake, wakati wataalam hao walipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa umeme wilayani humo.

Naibu Katibu Mkuu Nishati, awataka PURA kufanya kazi kwa weledi



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli, (PURA), Charles Sangweni, (aliyesimama) akitoa maelezo juu ya utendaji kazi wa Mamlaka hiyo wakati wa kikao cha Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja na wafanyakazi wa mamlaka hiyo kilichofanyika Oktoba 26, 2020 jijini Dar es Salaam.

Na Zuena Msuya, DSM

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja amekutana na watumishi wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli, (PURA) ili kujadili mambo mbalimbali kuhusu utendaji kazi wa Taasisi hiyo ambayo ni mpya na kuwataka kufanya kazi kwa weledi.

Mhandisi Masanja alisema hayo wakati wa kikao chake cha kwanza

na watumishi wa mamlaka hiyo, kilichofanyika Oktoba 26, 2020 jijini Dar es Salaam kwa kushirikisha baadhi ya viongozi waandamizi wa Wizara ya Nishati.

Katika kikao hicho, Mhandisi Masanja aliwataka watumishi wa taasisi hiyo kufanya kazi kwa weledi na kujituma kwa kuzingatia umuhimu wa kuwepo taasisi hiyo kwa maendeleo na uchumi wa nchi.

“PURA licha ya Taasisi yenu kuwa changa na mpya, watumishi wachache, wengi wao

wakikaimu nafasi mbalimbali za uongozi ni vyema sasa mkafanya kazi kwa kujituma na weledi na muonyeshe uwezo wenu wa hali ya juu ili kuthibitisha na kuuonyesha umma pamoja na mamlaka zilizoridhia kuanzishwa kwa taasisi hiyo kuwa PURA ni kitu muhimu kwa taifa letu”, alisema Mhandisi Masanja.

Viongozi Wakuu wa Wizara ya Nishati, walioshiriki kikao hicho ni pamoja na Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi,

Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Raphael Nombo na Makamishna wasaidizi kutoka idara ya Mafuta na Gesi.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa PURA, Charles Sangweni alitaja Majukumu ya PURA kuwa yamegawanyika katika makundi makuu matatu ambayo ni kuishauri Serikali juu ya masuala mbalimbali yahasuyo

Naibu Katibu Mkuu Nishati, awataka PURA kufanya kazi kwa weledi

INATOKA UK.

15

Utafutaji, Uendelezaji na Uzalishaji wa Mafuta na Gesiasilia.

Pia kusimamia na kudhibiti shughuli zote zinazohusiana na Mkondo wa Juu wa Petroli pamoja na kusimamia utekelezaji wa mradi wa kuchakata Gesiasilia kuwa katika mfumo wa kimiminika LNG (Liquefied Natural Gas Project).

Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) iliundwa kupitia kifungu namba 11, cha Sheria ya Petroli ya mwaka 2015: Katika kuhakikisha



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati) akizungumza na wafanyakazi wa mamlaka ya udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli wakati wa kikao chake na mamlaka hiyo juu ya utendaji kazi wa taasisi hiyo, kilichofanyika Oktoba 26, 2020 jijini Dar es Salaam. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli, (PURA), Charles Sangweni na kushoto ni Kamishna wa Petroli na Gesi, Wizara ya Nishati, Adam Zuberi.



Kamishna wa Petroli na Gesi, Wizara ya Nishati, Adam Zuberi (kulia) akizungumza na wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Petroli wakati wa kikao cha Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (hayupo pichani), katikati ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Wizara ya Nishati, Raphael Nombo. Kikao hicho kilifanyika Oktoba 26, 2020, jijini Dar es Salaam.

kuwa majukumu ya PURA yanatekelezwa, mchakato wa kuanzisha PURA kitaasisi uliendelea, ambapo Februari, 2016, Wizara ya Nishati na Madini (wakati huo) iliunda Kamati Maalum (PIC) ya Kuratibu mchakato wa kuanzisha PURA.

Mwezi Januari 2017, Waziri wa Nishati aliteuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu ili kubeba jukumu la kuiongoza PURA kwa kutumia kamati hiyo maalum, na Aprili, 2017, Bodi ya PURA iliteuliwa baada ya uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi uliofanywa na Rais Dkt. John Magufuli, tarehe 21 Aprili 2017.

Hatimaye Novemba 5, 2018, Rais Dkt. John Magufuli aliidhinisha Muundo wa PURA, na 2019.



PURA, STAKEHOLDERS TO WORK HAND IN HAND IN ENHANCING LOCAL PARTICIPATION IN THE UPSTREAM PETROLEUM ACTIVITIES

By Ebeneza Mollel

In an effort to ensure no stakeholder in Tanzania local content space is left behind, the Petroleum Upstream Regulatory Authority (PURA) is set to conduct local content consultative meetings on regular basis for the sole purpose of creating interactive forum for stakeholders to meet and deliberate on local content development in Tanzania upstream oil and gas sector.

Speaking at the first, one of a kind local content consultative meeting organized by PURA on 9th October 2020, the Authority Head expounded that the development of local nationals to actively and fully participate in the oil and gas sector, particularly in the upstream segment of petroleum value chain requires a joint, collaborative and coordinated effort between the Government, industry players and other relevant stakeholders. "It is abundantly clear that for local content objectives to be realized, there is a dire need for all players to work hand

in hand, to establish sort of yin and yang relationship unless otherwise, the spasmodic individual effort put forth will barely bear fruit", stressed the Authority Head in a hearty voice during that meeting attended by representatives from Ministry of Energy, National Economic Empowerment Council (NEEC) and Petroleum Exploration and Production Companies operating in Tanzania including Tanzania National Oil Company (TPDC).

Delivering a presentation in that meeting, the Local Content Lead (LCL) from PURA hinted that the Authority is now at a rudimentary stage in the drafting of the Upstream Petroleum Local Content Guidelines and that once the draft is finalized it will be shared with all stakeholders for their comments. To put some flesh on the bones of the Guidelines, the LCL further stated that the Guidelines will provide succinctly clear local content reporting templates which will bring about congruency and consistency in local content

performance reporting across industry players unlike now when there is no standardized templates. As a cherry on top, the LCL went on explaining that the Authority plans to establish a Common Qualification System (CQS), the tool that will be used to register and pre-qualify capable local suppliers and service providers in the country willing to participate in the upstream petroleum activities.

Representatives attending the meeting showered PURA with praise for getting off on the right foot in initiating local content consultative meetings for such meetings are critically important platforms for them to contribute ideas towards local content development in the country. "This is a lofty, commendable initiative. Massive congratulations to PURA. Being a Regulator does not necessarily mean policing players, waiting for them to defy the law or run afoul so as to penalize them. Regulatory roles go above and beyond lurking around like a watchdog waiting to

teach some lesson those who fail to comply with the regulatory requirements and those who deliberately flout the rules. The roles, I believe, include amicably engaging players for their opinion on how best regulations can be implemented and turning a listening ear to the hurdles, stumbling blocks, red tapes and challenges facing them", emotionally commented on one of the representatives from exploration and production companies.

Upon making sure PURA effectively regulate the implementation of local content requirements as stated in the Petroleum Act, 2015 and the Petroleum (Local Content) Regulations, 2017, the Authority has gone ahead to establish a fully-fledged, functional Local Content Unit (LCU) solely dedicated to local content and stakeholders' engagement. This step is major and expected to significantly contribute towards the realization of local content objectives particularly in the upstream part of the petroleum value chain.

JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



Fika Ofisi ya Mawasiliano,
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
Nukushi +255-26-2320148

 www.nishati.go.tz

 [Wizara ya Nishati](#)

 [@Nishati2017](#)

 [wizara_ya_nishati_tanzania](#)

 [Wizara ya Nishati](#)